



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 04 Machi, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

150. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, baadhi ya shehia za jimbo la Pandani ikiwemo Mzambarauni, kulikuwa na mchakato wa kufunguliwa akaunti za NMB za wananchi kwa kuilipia TZS 10,000/- kila moja kwa ahadi kutoka Serikalini ya kuingiziwa fedha za Maendeleo ya Vijana kutoka ughaibuni jambo ambalo hadi sasa halijafanyika.

- (a) Je, Serikali ilibariki zoezi hilo.
- (b) Je, zoezi hilo lilifikia wapi na wananchi katika shehia wamefaidikaje.
- (c) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi waliofuata maagizo hayo ya Serikali na kutotimiziwa ahadi waliyopewa.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

11. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIR (Jimbo la Uzini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Usajili wa vilabu vya mpira wa miguu kwa ajili ya kushiriki ligi na usajili wa wachezaji ni bei kubwa ukilinganisha na uwezo wa vilabu.

Je, ni lini viwango vya bei ya usajili vitashuka.

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

77. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kojani kina ukosefu wa mtaalam wa mashine ya “Ultra Sound”.

Je, ni lini Serikali itampeleka mtaalam wa fani hiyo.

79. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Kwa kuwa watumishi wa afya katika Kituo cha Kojani hulazimika kufanya kazi katika muda wa ziada kutokana na wingi wa kazi pamoja na mahitaji ya huduma ya afya siku hadi siku. Na kwa kuwa malipo ya muda wa ziada “overtime” ya watumishi huchelewa sana kulipwa.

Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha malipo hayo kuchelewa.

81. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Kwa muda mrefu wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakikabiliwa na changamoto za gharama za matibabu hasa kwa wale wagonjwa ambao wanawajibika kupelekwa katika hospitali za Tanzania Bara. Aidha, kwa wakati tofauti Serikali imekuwa ikieleza nia yake ya kuanzisha bima ya afya ili kukabiliana na changamoto hizo.

- (a) Kwa kuwa huduma za bima ya afya ni muhimu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha huduma hiyo.
- (b) Zipo habari kwamba utaratibu na Serikali kupeleka wagonjwa nchini India umesimamishwa. Je, hili ni kweli na nini chanzo cha hatua hizo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

92. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar imesaidia sana kuwapatia fedha watumishi wa umma kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu.

- (a) Je, ni sababu gani hupelekea watumishi ambao hawajakopa kukatwa mishahara yao kwa ajili ya kulipa deni la Bodi.
- (b) Je, fedha zinazokatwa kwa makosa, baada ya muda gani wanarejeshewa wenyewe.
- (c) Je, inachukuwa muda gani mkato huo huo uliofanyika kwa makosa kusitishwa.

158. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni jambo jema kwamba Serikali imekuwa ikitoa miongozo juu ya uvaaji wa sare za skuli. Hata hivyo, baadhi ya masharti ya vazi rasmi la wanafunzi imekuwa ni kikwazo kwa baadhi ya watoto na mara nydingi huwa hawalimudu.

- (a) Je, Serikali imeridhia wanafunzi kufukuzwa skuli na kurejeshwa nyumbani pindi wakishindwa kuvali viatu vya buti.
- (b) Je, Serikali ina utaratibu wowote wa kuwapatia sare watoto wanaotoka familia zisizojimudu.
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha sare zote vikiwemo viatu vya wanafunzi vinazalishwa nchini ili kuibua hisia za uzalendo kwa watoto.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

40. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya kila linalowezekana ili kuhakikisha kuwa maendeleo yanawafikia wananchi wake popote walipo kwa kujenga barabara za viwango ili kurahisisha harakati mbali mbali za maisha, sambamba na kupanga bajeti na kuzifanyia ukarabati pindipo kunapotokea hitilafu ya kubomoka.

- (a) Je, Wizara inalifahamu tatizo la kuwepo kwa mashimo katika barabara ya Kilindini Micheweni ambapo sasa inaleta usumbufu kwa wasafiri wanaotumia barabara hiyo.
- (b) Je, kuna hatua au vigezo gani ambavyo vinatumia na Serikali mpaka barabara iweze kufanyiwa ukarabati pindipo ikianza kuharibika.

**Zanzibar,
04 Machi, 2022.**

**(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA.**